BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Saba – Tarehe 06 Disemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali ya 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo

.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

34. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na msongamano mkubwa kwa wananchi wanaotaka huduma za vyeti vya vizazi na vifo, licha ya msongamano huu utaratibu wa wananchi hao kulipia benki umekuwa ukiwaletea usumbufu hasa kwa wale wanaotoka vijijini, hasa kwa vile malipo mengi hayazidi shs. 5,000/-

(a) Je, hivi Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kubadilisha utaratibu wa malipo ili kupunguza usumbufu kwa wananchi.

(b) Kwa kuwa nchi nyingi zimeanza kutumia utaratibu wa mashine za EFD, Je, nasi hatuoni kwamba wakati umefika wa kutumia mashine hizo.

122. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa viongozi wa Serikali za Mitaa (masheha) ni watumishi wa umma kuanzia siku ya uteuzi wao. Na kwa kuwa viongozi hawa wanamajukumu makubwa ya vijiji vyao na Serikali kuu kwa ujumla.

(a) Je, hatuoni kuendelea kuwalipa mshahara kima cha chini ni kuwaonea na muda wao wa kazi ni masaa 24 tofauti na watumishi wengine.

(b) Je, ni lini Serikali itaandaa na kuwapatia vitambulisho vya kazi zao watumishi hawa kama ilivyo watumishi wengine ili kuwaondolea usumbufu wakati wanapohitaji huduma.

(c) Je, ni lini Serikali itawapatia huduma za usafiri utakaorahisisha kazi zao za kila siku.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

103. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake za kuleta maendeleo chini ya uongozi imara wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sekta ya Wizara ya Habari ni muhimu kwa vyombo vya Habari. Hata hivyo, inaonekana bado kuna tatizo la watangazaji na mafundi katika lugha za kigeni hasa lugha ya kichina, kifaransa na kiarabu ukiachia kiingereza kama lugha ya taifa kwa mazoea tuliyonayo.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasomesha watangazaji wetu wazifahamu lugha hizo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasomesha watangazaji wetu katika lugha hizo.

(c) Je, Serikali haioni umuhimu kwa sasa kutoa kipaumbele kwa watangazaji wetu tutakaowaajiri kutoa kipaumbele cha lugha za kigeni angalau wawili kwa kila lugha.

Wizara ya Fedha na Mipango:

15. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Wananchi wa Mbuyu Tende walioko Matemwe wamekuwa na kilio cha muda mrefu na cha siku nyingi cha Mwekezaji kuvamia maeneo ya makaburi na kujenga hoteli ya kitalii.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ya kumaliza tatizo hilo.

(b) Je, kwanini Mwekezaji huyo anaruhusiwa kujenga kitega uchumi katika eneo la makaburi wakati Serikali imetenga maeneo maalum ya uwekezaji.

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya watendaji waliotoa vibali vya ujenzi katika eneo la makaburi.

16. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Wateja wa Benki ya FBME Tawi la Zanzibar, kwa muda mrefu wamekuwa na kilio cha haki yao ya msingi kabisa na kupata hasara kubwa kwa kukwama kwa fedha zao na kuna taarifa baadhi ya wateja wamo ndani ya chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi.

(a) Je, SMZ imefanya jitihada gani ili kuwasaidia wananchi wake juu ya kadhia hiyo iliyotokea.

(b) Je, Waziri wa Fedha wa SMZ amewahi kukaa na Waziri wa Fedha wa SMT kumueleza kero hii ya wananchi wetu.

(c) Je, kitendo cha kukaa kimya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) haioni imeshindwa wajibu wake na imefika wakati wawajibishwe.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

81. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Je, ni hatua gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikia katika suala zima la utafiti wa mafuta na gesi.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

64. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake za kuleta maendeleo Zanzibar na wananchi kwa ujumla kupitia Wizara ya Elimu. Lakini katika sekta ya elimu nimeona kwamba skuli zote zimejikita katika kusomesha masomo ya kawaida. Wakati katika sekta nyengine za vipaji kama vile michezo yenye ajira kubwa kwa kwetu Zanzibar bado haijajikita kwenye michezo hiyo ya fani mbali mbali za kujiajiri. Hali hii inapelekea wanafunzi wanapomaliza masomo yao kusubiri ajira kutoka serikalini tu.

(a) Je, Zanzibar ina skuli ngapi zenye fani maalum na vipaji mbali mbali kwa wanafunzi ili watakapomaliza wenye vipaji hivyo wajiajiri wenyewe ukiachana na skuli za masomo ya kawaida.

(b) Je, Zanzibar haioni sasa imefika wakati wa kuanzisha skuli maalum za fani na vipaji mbali mbali kwa wanafunzi wadogo wadogo ili kuwawezesha kitaaluma katika fani hizo.

(c) Je, pale inapoonekana vipaji vya wanafunzi katika michezo mbali mbali, Serikali huchukuwa hatua gani katika kuviendeleza vipaji hivyo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

41. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa misitu yetu inavyo vivutio mbali mbali ambavyo wageni wetu kutoka nchi mbali mbali hupenda kutembelea na kupiga picha ambazo nyengine huwa ni kwa ajili ya biashara au maonesho au wengine kwa ajili ya mfumo na tafiti mbali mbali.

(a) Je, ni tozo la kiasi gani na mpangilio wa tozo hilo ambazo hutozwa wageni wanapopiga picha katika misitu yetu ya uhifadhi.

(b) Je, kwa mwaka 2017/2018 hadi kufikia mwezi Oktoba kwa Pemba na Unguja Serikali ilipata kiasi gani cha fedha kupitia vivutio vya misitu hiyo.

(c) Je, wageni waliotembelea misitu hiyo wengi wao walitoka nchi gani na walivutiwa na vitu gani ambavyo walipendekeza vihifadhiwe ambavyo ni adimu ulimwenguni.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

92. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikijitahidi kuweka vituo vya mafunzo ya amali “Vocational Training Centre” nchini katika kutekeleza Ilani ya CCM ya 2015.

Je, Serikali imejiwekea utaratibu gani wa kutayarisha mfuko maalum utaowawezesha vijana hao kupata mtaji ili kujiajiri kupitia elimu waliyopata.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

27. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Tarehe 29/06/2018 katika Kikao cha kuwasilisha utekelezaji wa Mpango kazi wa Wizara wa kila robo mwaka (Bango Kitita), Wizara hii imeagizwa kununua vifaa vya ujenzi wa barabara ili kukamilisha matengenezo na ujenzi wa barabara mbali mbali kama vile Ole-Kengeja (7Km) n.k. Hata hivyo, mahitaji ya fedha za ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo ni doza, greda, kijiko, gari n.k ni makubwa na hayakukasimiwa fedha katika bajeti ya mwaka 2018/2019.

(a) Je, gharama za ununuzi wa vifaa hivyo ni kiasi gani.

(b) Je, vifaa hivyo vitanunuliwa kwa fedha zipi wakati Baraza hili halijapitisha kwenye bajeti ya Wizara.

(c) Je, Serikali haioni kuwa kutoa maagizo ya ununuzi wa vifaa hivyo nje ya bajeti kunaonesha udhaifu wa mipango yetu ambayo haiakisi bajeti husika.

28. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Imeonekana hapa nchini kwetu kuna tofauti za bei za nauli za usafiri kama vile ndege au boti kwa wageni ambao wanalipa tofauti na wazawa. Utaratibu huu haupo duniani kwani wageni na wazawa wanalipa nauli ile ile bila ya ubaguzi wowote.

Je, tofauti ya nauli za usafiri kwa wageni na wazawa zinapangwa kwa sheria na kanuni zipi.

III. HOJA ZA SERIIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

.

Zanzibar,
06 Disemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.